TANGAZO LA SERIKALI Na. 138 la tarehe 28/2/2025

SHERIA YA USHURU WA BIDHAA,
(SURA YA147)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128)*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWA MAGARI MATATU YANAYOINGIZWA NCHINI NA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII KWA AJILI YA MRADI WA KUTATUA MIGONGANO BAINA YA WANYAMAPORI NA BINADAMU YA MWAKA 2025

Jina na kuanza kutumika

**1**. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwa Magari Matatu Yanayoingizwa Nchini na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Ajili ya Mradi wa Kutatua Migongano baina ya Wanyamapori na Binadamu ya Mwaka 2025, itaanza kutumika kuanzia tarehe 20 Januari, 2025

Msamaha

**2**. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3, na masharti mengine yoyote yanayoweza kuainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kiasi chote cha ushuru wa bidhaa kinachotakiwa kulipwa kuhusiana na magari matatu yaliyoainishwa kwenye jedwali, yanayoingizwa au kununuliwa ndani ya nchi, kabla ya kibali cha forodha na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mradi wa Kutatua Migongano baina ya Wanyamapori na Binadamu umesamehewa.

Masharti

**3**. Msamaha wa kodi unaotolewa chini ya Amri hii utafika ukomo na ushuru utadaiwa na utatakiwa kulipwa kana kwamba msamaha chini ya Amri hii haukutolewa, iwapo magari husika yatatumika kwa matumizi tofauti au yatahamishwa, kuuzwa au kwa namna yoyote atapewa mtu mwingine asiyestahili kufaidika na faida zinazotolewa chini ya Amri hii.

Ukomo

**4**. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utafika ukomo tarehe 19 Mei, 2025.

JEDWALI

(Imetengenezwa chini ya aya ya 2)

MAGARI

| Na. | Maelezo | Idadi | Namba ya Chassis | Namba ya Injini | Mahali |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Land Cruiser 76 Hardtop 10-Seater, 5 Doors | 01 | JTEEB71J70F032940 | 1HZ-1085921 | Limeingizwa |
| 2 | Land Cruiser Prado BX 2.8L Turbo Diesel Auto 7 Seats | 01 | JTEARICAJ50K008288 | 1GD-9361406 | Limeingizwa |
| 3 | Land Cruiser Prado BX 2.8L Turbo Diesel Auto 7 seats | 01 | JTEARCAJ50K008338 | 1GD-9363061 | Limeingizwa |

Dodoma,
18 Februari, 2025

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
*Waziri wa Fedha*